## Sura ya 2 – Mto utiririkao

**Kusafisha**, **kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi wa Yesu**, **kueneza Injili**, **kuifikia** "bahari ya chumvi" ya wanadamu. Ezekieli 47:1-12

**Makusudi ya Mungu ni kuwafikia wanadamu waliopotea.**
**Kwa njia gani?**


Ezekieli 47:1-12: Picha aliyoonyeshwa Ezekieli ni ya Hekalu la Mungu na mto unaotoka katika hekalu hilo. Mungu aliongea na Ezekieli na kumwonyesha kwamba huu ulikuwa Mto wa Uzima unaotiririka kutoka kwa Mungu hadi kwenye bahari ya chumvi na kuingia katika maji machafu yaliyooza. Mto huu utayaponya maji hayo na kuyafanya hai.

Kwa kawaida bahari katika Biblia, humaanisha bahari ya wanadamu waliopotea. Mungu alikuwa akimuonyesha Ezekieli kwamba njia pekee ya kuwafanya wanadamu waweze kuishi, ni kwa kuguswa na Mungu, kwa njia ya kitu kinachoitwa **Mto** unaotiririka kutoka katika uwepo wake mwenyewe.

Katika Yohana 7:38 imeandikwa hivi, "Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, **Mito** ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake."

Hekalu liko wapi leo? Katika 1 Wakorintho 6: 19-20 tunaambiwa hivi; "Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu."


**Mto unatiririkia ndani ili kukusafisha – Mto unatiririkia nje ili kuuokoa ulimwengu uliopotea**



Mungu WEWE Ulimwengu uliopotea

**Tunahitaji uwepo wa Mungu utuweke huru na kutusafisha, ili tuweze kufanya aina yoyote ya huduma na hata kuomba maombi yaletayo matokeo.**

**Tunahitaji kujua kwamba kuna maadui wanaotaka kumzuia Mungu asionekane kwamba ni kweli yupo pamoja nasi.**



Maadui zetu huja kwetu kwa njia kuu tatu

*Utashi wetu –*
*Akili zetu –*
*Hisia zetu –*
**Hushambuliwa na Mwili, Ulimwengu na Shetani**

Swali
**Tunawezaje kuwashinda maadui hawa ili tuweze kuingia katika uwepo wa Mungu na kuwa na USHIRIKA naye?**

Jibu
**Mungu ameishatupatia ushindi dhidi ya maadui wote! Njia ya kuingia katika uwepo wake ilipatikana pale msalabani wakati pazia lilipopasuka toka juu hata chini – Marko 15:38. Sasa ni kazi yetu kushirikiana naye. Tunapaswa kubeba msalaba wetu – huo utatupatia ushindi!**

Katika Luka 9:23-25 Biblia inasema, "Akawaambia wote, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na **ajikane** mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya **nafsi** yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza **nafsi** yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha. Kwa kuwa yamfaa nini mtu kuupata ulimwengu wote, kama akijiangamiza, au kujipoteza mwenyewe?

Neno hilo **nafsi** katika Luka 9 linamaanisha utashi, akili na hisia. Neno **kukana** linamaanisha kukataa kitu fulani.

**Ufunguo wa kupata uzima tele na kupokea baraka kutoka kwa Yesu, hii ikiwa ni pamoja na uwepo wake, ni kukamilisha agano la damu kwa kubeba msalaba wetu.**

Wengi wetu tunajua kazi nzuri sana, yenye uweza mkuu, iliyohusisha kila kitu, ambayo Yesu aliifanya juu ya msalaba wa Kalivari, jinsi alivyomwaga damu yake kwa ajili ya dhambi zetu, na kufufuka katika wafu ili kutupatia uzima. Hatuwezi kuongeza chochote juu ya hayo. Hata hivyo, ili tuweze kunufaika na kazi hiyo, hatuna budi pia kufa. Lazima tubebe msalaba wetu, tujikane wenyewe na kumfuata. Ni lazima tuiangamize nafsi yetu.

Uhusiano na USHIRIKA wetu na Mungu umejengwa juu ya msingi wa agano la damu. Kwa wengine jambo hilo linaweza kuonekana geni. Jambo hilo linaweza kulinganishwa vizuri zaidi na ndoa. Watu wengi sana wana ufahamu usio wa kibiblia kuhusu uhusiano huu wa agano la damu. Hebu jiulize swali hili: Je, ungeweza kujadiliana na mchumba wako kuhusu uhusiano mwingine wa kimwili unaoruhusiwa kuwa nao na wanawake wengine baada ya ndoa?

**Agano la damu huchochewa na vifo VIWILI; cha Yesu na chako!**


**Ni kitu gani muhimu sana kuhusu agano la damu?**



Katika kitabu cha 1 Petro 1:18-19 tunasoma maneno yafuatayo: “Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa **damu** ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo.”

Katika Mambo ya Walawi 17:11 tunasoma pia maneno yafuatayo: “Kwa kuwa uhai wa mwili u katika hiyo damu; nami nimewapa ninyi hiyo damu juu ya madhabahu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu; kwani ni hiyo damu ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi.”

**Maisha ya kiroho yanaweza kubadilishana na ile sheria ya mbadala. Agano la damu hubadilisha urithi wa familia yako.**





Kimsingi, hii ina maana kwamba watu wanaweza kuzaliwa katika familia fulani, na katika familia au ukoo wao huo, wakapokea baraka na laana kama urithi wao. Hata hivyo, baraka na laana zinaweza kubadilishwa. Makabila kadhaa katika bara la Afrika, na pia katika utamaduni wa Wahindi wekundu na katika jamii nyingine za Asia, yamekuwa kila wakati yakitafuta njia za kubadilishana na watu wengine baraka na laana.

Kabla ya kuumbwa kwa dunia, Mungu alikuwa amepanga kwamba Yesu asulibiwe kulingana na Roho wa UZIMA, na hii ina maana kwamba ile kanuni ya mbadala ilikuwa ikitenda kazi hata kabla mwanadamu hajaumbwa (Ufunuo 13:8).

**Ili agano la damu liweze kweli kufanya kazi, ni lazima kila upande unaohusika umwage damu, au ni lazima viwepo vifo viwili au misalaba miwili. Lazima utu wetu wa kale ufe na kisha tujikabidhi sisi wenyewe na vyote tulivyo navyo kwa Yesu. Jambo la kufurahisha ni kwamba hata Yesu mwenyewe ametoa yote aliyo nayo na kujitoa mwenyewe kwetu!**

**Tunapounganisha msalaba wa Yesu na msalaba wetu tunakuwa tumeunganishwa na Mungu...**
**na Nguvu hutokea!**





**Kila wakati kunakuwa na misalaba miwili inayopaswa kuungana ili kufanya agano la damu.**

**Hema ni alama yenye nguvu ya misalaba miwili inayofaa kutumiwa kama mwongozo wa maombi. Itatusaidia kubeba msalaba wetu na kutuingiza katika uwepo hasa wa Mungu na kuwa na USHIRIKA naye!**

"Agano la Kale linatuambia jinsi wateule wa Mungu walivyoishi duniani. Kwanza, Hema lilitumika kama kituo cha makabila 12; baadaye Hekalu ndilo lililokuwa kituo chao. Kituo cha Hekalu kilikuwa Sanduku. Hema, Hekalu na Sanduku ni aina mbalimbali za Kristo. Kadri wana wa Israeli walivyokuwa na uhusiano mzuri na Hema au Hekalu walipata ushindi, na hakuna taifa lililoweza kuwashinda. Ingawa wana wa Israeli walikuwa hawajui kupigana, waliwashinda maadui zao wote waliokuwa wamejifunza jinsi ya kupigana. Lakini wakati walipokuwa na tatizo kuhusiana na Hema au Hekalu, walichukuliwa utumwani. Haikusaidia kitu kuwa na wafalme wenye nguvu au hekima kubwa, kitu muhimu kilichoangaliwa ni iwapo wamelikosea sanduku la maskani au hekalu. Walipotoa kipaumbele kwa Mungu, ushindi ulikuwa wao. Ndivyo ilivyo hata leo. Tukiuzingatia ushindi wa Kristo, sisi pia tutapata ushindi."

Dondoo kutoka katika kitabu kiitwacho "God's plan and the Overcomers" (Mpango wa Mungu na washindaji), kilichoandikwa na Watchman Nee

**Unavyoendelea kuwa na ushirika na Mungu, jaribu kujiona kana kwamba unatembea katika Hema kama jinsi makuhani wa Agano la Kale walivyofanya.**


Tunaanzia hapa
Tunatembea mpaka hapa na kubeba msalaba wetu
Tunaishia hapa katika uwepo wa Mungu
Hema
Ua wa nje
Patakatifu
Beba msalaba wako
Patakatifu pa Patakatifu
Mahali tunapokutana na Mungu katika uwepo wake
Madhabahu ya shaba
Msalaba wa Yesu
Birika la Shaba
Neno
Kinara cha Taa
Nia (Akili)
Madhabahu ya kufukizia
Hisia
Meza ya Mikate ya Wonyesho
Utashi
Sanduku
Kiti cha Rehema
Damu
Mana
Fimbo ya Haruni
Sheria
Mapazia
Kwanza: Msalaba Wake

## Kwanza: Msalaba Wake

Kwa ajili yako

Nyakati za Agano la Kale, kila mwaka Wana wa Israeli walikuwa wakiadhimisha Siku ya Upatanisho ijulikanayo kama "Yom Kippur". Dhambi za wana wa Israeli zilikuwa zikishughulikiwa katika siku hii moja tu ya mwaka, wakati kuhani mkuu alipojiandaa kuingia katika Hema kwa niaba ya wana wa Israeli kwa ajili ya dhambi zao.

Pale kwenye madhabahu ya Shaba, katika ua wa nje, kulikuwa na mbuzi wawili. Mmoja alifungwa kitambaa chekundu shingoni mwake kuonyesha kwamba atachinjwa kwa ajili ya damu. Mwingine alifungwa nje ya lango kuonyesha kwamba angekuwa Azazeli. Mbuzi wa kwanza alichinjwa madhabahuni na damu yake ilipelekwa na kuhani patakatifu pa patakatifu ambapo aliitoa kwa kufukizia kando ya madhabahu ya kufukizia (mahali pa sifa). Uvumba ulipokuwa ukiungua, ulisababisha moshi ujae patakatifu pa patakatifu, na hiyo iliwakilisha (na kuleta hasa) uwepo wa Mungu. Kuhani alinyunyiza damu juu ya Kiti cha rehema mara moja na pia alinyunyiza damu mbele ya Kiti hicho mara saba. Nje ya marago, kila mtu alilala kifudifudi wakati yote hayo yalipokuwa yakiendelea. Hakuna mtu aliyeona chochote kilichokuwa kikifanyika, na hiyo ilimaanisha kwamba dhambi zao zilisamehewa kwa mwaka mzima.

Pili, kuhani aliporudi na kubadili nguo zake, aliweka mikono yake juu ya mbuzi mwingine, Azazeli, kuashiria kwamba dhambi zote zimehamishiwa juu ya kichwa cha mnyama huyo. Kulikuwa na mtu aliyechaguliwa kumpeleka mbuzi huyo jangwani mahali pasipokaliwa na watu na kumwacha sehemu ambayo hawezi tena kurudi au kutoroka. Mtu huyo kwa mfano, alimpeleka mbuzi yule hadi kwenye bonde lililozungukwa na miamba na majabali na kisha mbuzi yule aliteremshwa chini ili asiweze kutoroka(Mambo ya Walawi 16:21-22).

Sasa kuhani alipoweka mikono yake juu ya mbuzi aliye hai, ili kuanza sehemu ya pili ya ibada, aliungama dhambi zote za wana wa Israeli. Alisema, “Bwana, weka dhambi zangu na za wana wa Israeli juu ya kichwa cha mbuzi huyu. Haya, we mbuzi, ondoka." Mbuzi yule alipokuwa akipelekwa nje ya marago, watu wote walisimama na kushangilia. Watu wote na hata watoto waliweza kuona tukio hilo na


kufahamu. Azazeli ni mfano wa Yesu aliye Azazeli wetu, aliyeshushwa chini hata kuzimu kwa ajili yetu huku dhambi zetu zikiwa juu ya kichwa chake. Alichukua dhambi zetu na kuziondoa kabisa, zisionekane tena au kurudi. Zaburi ya 103:12 inasema "Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, ndivyo BWANA anavyowahurumia wamchao." Katika kitabu cha Mika 7:19 tunasoma pia maneno haya "Atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari."

Katika kitabu cha Waebrania 9:12-14 tunapata pia maneno yafuatayo "wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kutusafisha mwili; basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?"

# Pili: Msalaba Wetu



## Hema




Yesu aliposema kwamba ni lazima tujikane, tuiangamize nafsi kwa ajili yake, nk., alikuwa na maana kwamba tunapaswa kuikana au kuiambia nafsi "hapana".

Nafsi yetu ina sehemu tatu: Utashi, Nia (Akili) na Hisia. Patakatifu panawakilisha ile sehemu ya utu wetu, yaani nafsi.Sehemu hiyo ilikuwa na na aina tatu za fanicha au samani zinazowakilisha utashi wetu, Akili na Hisia (Angalia mchoro huo hapo juu). Kwa hiyo tunapoziambia sehemu hizi "hapana" na kusema "ndiyo" kwa yale aliyo nayo Mungu, huku ndiko kuubeba msalaba wetu.

*Utashi wetu-*
*Akili zetu-*
*Hisia zetu-*
**hushambuliwa na Mwili, Ulimwengu na Shetani**

**Sasa tutasafiri hadi kwenye sehemu zote hizo tatu wakati wetu wa maombi na pia tutaendelea na safari na kuwapita maadui zetu hadi katika uwepo wa Mungu!**

## "Mto Utiririkao"
## (Mwongozo wa Maombi ya Kila Siku)

### Kusafiri hadi katika Uwepo wa Mungu

Maelekezo:

1. Soma kwanza kurasa 7 za mwanzo, na kisha zisome tena angalau mara moja kwa mwezi. Halafu kila siku, anzia ukurasa huu, na uwe na muda wa kuwasiliana na Mungu angalau kwa dakika ishirini.

2. Utakapoanza na hema ya kukutania, mgongo wako unapaswa kuielekea dunia huku uso wako ukimwelekea Yesu. Hii ni muhimu kwa sababu Roho Mtakatifu hawezi kukaa na wewe iwapo unaelekea mahali pabaya. (mwelekeo wa kiroho, Matendo ya Mitume 26:18)

3. Nenda hadi kwenye kila "kituo" ushughulike na somo hilo katika hali ya maombi pamoja na Bwana. Tafuta katika Biblia baadhi ya maandiko. Uwe macho kuhusu maeneo yanayohitaji toba, kwa sababu jambo hili ni moja kati ya michango yetu mikubwa, wakati huu tunapokuwa na ushirika na Mungu.

4. Ni vema ukipitia vituo hivi vyote kwa wakati mmoja. Unaweza kufanya hivyo kwa DAKIKA ISHIRINI. Hata hivyo, kama huna muda wa kupitia utaratibu huu wote kwa mkao mmoja, usikate tamaa. Badala yake, anza utaratibu huu asubuhi, na umalize angalau hatua moja. Kisha endelea na hatua ya pili wakati wa chakula cha mchana. Kama unahitaji, endelea siku inayofuata. Hatimaye ishi maisha yanayofuata utaratibu huu na itakuwa kawaida kwako kukaa katika uwepo wake Mungu.

### Ua wa Nje

**Kituo cha kwanza: Madhabahu ya Shaba - Msalaba wa Yesu.**

**Msamaha**

**Madhabahu ya Shaba**

Agano la damu hubadili mabaya yote tuliyo nayo na kuweka mema yote aliyo nayo Mungu. Hata hivyo hatuwezi kupata msamaha wa dhambi bila kumfanyaYesu kuwa Bwana (Warumi 10:9-10).

Anza leo kuwa mkweli mbele za Yesu. Neno la Mungu katika 1 Yohana 1:9 linasema "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu

na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

Sehemu kubwa ya kubeba msalaba wako ni kuwa MKWELI KABISA mbele za Mungu. Unahitaji kuwa wazi kabisa na kumwambia kila kitu. Uwe na muda wa kuumimina moyo wako kwa Mungu kama jinsi ambavyo ungefanya kwa mtu ambaye ni rafiki yako sana! Biblia inasema katika 1 Yohana 1:7 kwamba "**tukienenda nuruni**, kama yeye alivyo katika **nuru**, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote." Yesu alisema katika Yohana 3:19 kwamba dhambi haina nguvu iwapo watu watakuja kwenye nuru pamoja na kweli, bila kujaribu kujificha gizani. Yesu hakufa kwa ajili ya visingizio vyetu. Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu!

**Unahitaji kutembea katika upendo, na ikitokea kwamba umefanya dhambi, kimbilia kwa Mungu, usafishwe.**

"Sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti"(Warumi 8:2). Tukimgeukia Mungu kila wakati, na kudumu katika hali ya uaminifu mbele zake, atatushindia makosa yetu na vikwazo.

**Angalia Mto Utiririkao Kiambatisho cha F ujitathmini mwenyewe kwa uaminifu.**

Kama hakuna dhambi zinazojulikana, basi kiri kwa kinywa chako maneno yaliyoandikwa katika Wagalatia 2:20 na 2Wakorintho 5:21.

## Kituo cha Pili: Birika: Neno la Mungu

### Birika la Shaba

Kwa kuwa sasa fahamu zetu ziko wazi na tunaweza kuwasiliana na

Mungu, hebu twende kwenye Neno. Neno linasema kwamba kuhani angekufa kama angejaribu kuingia patakatifu kabla ya kusimama kwenye birika. Hatuwezi kwenda katika uwepo wa Mungu bila kusafishwa na Neno la Mungu (Waefeso 5:26-27).

Birika litatuondolea uchafu wa dunia. Litakuwa pia kioo cha kutuhukumu, litatuletea katika akili zetu mambo tunayopaswa kurekebisha mbele za Mungu. Neno litahuisha nafsi zetu ili tuweze kufikiri kiroho na kuwa kinyume na maneno ya pepo yanayokuja katika akili au fahamu zetu.

Neno linatuambia pia kwamba Shetani amekwisha hukumiwa (Yohana 16:11). Hakikisha unasema maneno haya kwa sauti "Shetani umekwisha hukumiwa, umeshindwa!"

Tumia dakika chache katika Neno!

a. Tumia kitabu chako cha sala

b. Tumia kitabu chako cha "ISOB" au kitabu kingine cha kujifunzia Biblia.

c. Soma kitabu cha Mithali

d. Soma Zaburi sura moja au zaidi.

e. Soma vitabu vingine vinavyohusu Biblia au soma tu Biblia na umwombe Roho Mtakatifu akutafsirie. Soma Biblia yote kwa mwaka mmoja.

f. Sikiliza mafundisho au kanda za nyimbo zenye Neno la Mungu.

Kituo cha Tatu: Pazia la Kwanza: Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu.

**Pazia la kwanza: Kushukuru**

Kwa kuwa sasa umekaa katika Neno, unajua uko safi mbele za Mungu na kwamba Shetani amehukumiwa, basi unayo mengi ya kumshukuru Mungu! Hata kama huoni kwa haraka mambo ya kumshukuru Mungu jaribu kuyatafuta. Kama umeshindwa kuyapata, mshukuru kwa Neno lake linalosema kwamba unao ushindi ukiendelea kulishikilia Neno. Mshukuru pia Mungu kwa ahadi alizokuahidi ambazo bado hazijatimia katika maisha yako.

**Kituo kinachofuata kipo ndani ya Patakatifu**

**Hapa ndipo unapompa Yesu utashi au mapenzi yako na Yeye anakuonyesha mapenzi yake, unampa ufahamu wako na Yeye anakupa ufahamu wake, unampa hisia zako na Yeye anakupa hisia zake. Huku ndiko kuubeba msalaba wako, kujikana mwenyewe na kumfuata Yesu** (Luka 9:23)

**Utashi wako**

Meza ya Mkate wa Wonyesho

Badilisha haja za moyo wako (hata kama ni nzuri) kwa ajili ya mpango au mapenzi ya Mungu katika maisha yako. Weka chini matakwa na mipango yako na umwombe Mungu akuonyeshe mapenzi yake na mipango yake kwako.

Kila wakati Mungu huangalia utashi au mapenzi yetu; hii ndio maana ya mkate wa wonyesho. Mkate ni unga uliosagwa, ukachanganywa na mafuta na kuokwa motoni. Matakwa yetu na hamu zetu ni lazima kila wakati zitolewe madhabahuni zisagwe na kuchomwa. Hii ni sadaka maalum kabisa kwa Mungu, kwa kuwa ni utashi *wetu*, na yeye hawezi kutulazimisha wala kutuamrisha kufanya hivyo. Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu (Warumi 12:1-2).

Amua kusamehe hata kama hujisikii kufanya hivyo. Hii ni nafasi ya kutubu na kuacha njia za kidunia na kuzifuata njia za Mungu. Tunapoacha njia mbaya, tunapata nguvu za Mungu (Mdo 26:18 na 2 Kor 3:16).

**Badilisha tamaa za mwili, uwe na tunda la Roho. Tunda la Roho ni**: upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi (Wagalatia 5:19-23).

## Nia yako

### Kinara cha Taa cha Dhahabu

Badili nia au mawazo yako ya zamani uwe na nia ya Kristo. Katika 2 Kor 10:4-6 tunaambiwa kwamba vita viko katika mawazo na fikra zetu. Na kwamba ngome ni mawazo yetu. Mawazo haya hutufanya tuwe mbali na elimu ya Mungu. Kuna mengi ya kusema hapa kwa sababu mawazo yetu ni sehemu muhimu ya maisha yetu. Tunapaswa kuyaweka huru mawazo yetu. Kwa njia gani? Tulipokuwa watumwa wa dhambi tulitumia Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya ambao ni mawazo yetu. Sasa tunapaswa kutumia Mti wa Uzima ambao ni Neno la Mungu. Siwazi tena na kuamua, bali natumia akili zangu kwa sababu ni makusudi ya Mungu, na hiyo ndiyo kusikia na kutii! Hii pekee ndiyo itakayoangusha ngome katika akili zetu. Tukiuona utukufu wa Mungu kama Paulo alivyouona alipokuwa njiani kuelekea Dameski, hatuwazi tena, tunasema tu, “Bwana, unahitaji nifanye nini.”

Mara kwa mara pepo hutushitaki na kushambulia akili zetu kwa kutumia nusu ukweli. Katika Isaya sura ya 11 tunaambiwa kwamba Mungu hubadilisha maarifa yetu ya asili na kutuwekea yale ya Roho Mtakatifu, yaani Roho wa Bwana, hekima na ufahamu, shauri na uweza, maarifa na kumcha Bwana.

Tunahitaji mawazo au nia zetu zifanywe upya kwa Roho Mtakatifu na Neno la Mungu (Warumi 12:2). Wakati mwingine hatujui kuomba

jinsi itupasavyo. Katika Warumi 8:26 tunaambiwa kwamba tukiomba kwa lugha, tutaomba sawa sawa na mapenzi kamili ya Mungu. Kwa hiyo kila unapoomba kwa lugha utakuwa unaomba sawa sawa na Neno la Mungu na pia sawa sawa na mapenzi ya Mungu. Ile sehemu inayohusika na usemi au kunena, hutawala akili, na hivyo nia au mawazo yako hufanywa upya na kusawazishwa ili yaweze kuuambia mwili wako utende mapenzi ya Mungu.

## Hisia zako

### Madhabahu ya kufukizia uvumba

Badilisha hisia zako za zamani zilizosababishwa na mwili wako na ulimwengu, na nafasi yake ichukuliwe na tunda la amani, furaha, upendo, tumaini, nk. Hapa ni mahali pa dhabihu za sifa. Soma Zaburi 145-150 kwa sauti kubwa, kama hujisikii kumsifu Mungu moyoni mwako. Mungu anawatafuta watu wanaomwabudu katika Roho na kweli (Yohana 4:24). Kutoka katika mahali hapa pa sifa, Mungu atakutafuta na atahitaji kuwa pamoja nawe!

Mpatie hizo hisia ambazo umekuwa ukificha; labda ni machozi yako, labda ni kuinua kwako mikono, au labda ni kumfunulia tu hisia zako za kweli. Songa mbele, hakuna mwingine anayeangalia isipokuwa Yeye!

Mbele ya madhabahu hii kuna pazia linaloficha au kutenganisha patakatifu pa patakatifu na uwepo wa Mungu. Mungu anataka upite katika pazia hilo mara nyingi zaidi ya vile unavyohitaji. Atakusaidia kufanya hivyo. Hakuna mwanadamu wa kawaida anayeweza kuingia hapo bila kufa.

Pazia hili lilipasuka kutoka juu hata chini wakati Yesu alipokufa msalabani, akatuwezesha kuingia katika uwepo wa Mungu kwa damu yake, na kuonyesha kwamba kifo chake kimeondoa kizuizi kilichosababishwa na dhambi. Kizuizi hicho kilikuwa kinatuzuia kuingia katika uwepo wa Mungu. Msifu Mungu kwa ukweli huu.

Patakatifu pa patakatifu ni mahali aambapo hakuna mwanga au taa isipokuwa kwa ajili ya Mungu. Kuhani Mkuu aliweza tu kuingia hapa mara moja kwa mwaka, tena kwa masharti maalum. Ukweli ni kwamba madhabahu hii iliingia Patakatifu pa Patakatifu pamoja na Kuhani Mkuu mara moja kwa mwaka. Hii inaashiria kwamba kusifu kwako na kuabudu hakuishii hapa bali ni mlango wa kuingia katika uwepo wake, na mambo hayo huenda pamoja nasi.

**Sasa Mungu atakuvuta na kukupitisha katika pazia hadi Patakatifu pa Patakatifu - penye uwepo hasa wa Mungu**

**Sanduku la Agano**

Hili hapa Sanduku la Agano. Limefunikwa na Kiti cha rehema kilichonyunyiziwa damu. Tulihitaji rehema kwenye madhabahu ya shaba, yaani msalaba, mwanzoni kabisa. Lakini sasa katika uwepo wake kuna ufahamu mkubwa wa rehema yake na damu ya Yesu kwa namna ambayo Roho Mtakatifu pekee ndiye awezaye kukuonyesha. Rehema zake ni za milele. Ni kama haiwezekani kabisa kuandika rehema zake jinsi zilivyo, ni lazima mtu apate uzoefu wa rehema hizo.

Katika kila upande kuna malaika wakubwa wanaolinda kila kitu. Hapa pia hakuna nuru kabisa au taa isipokuwa kwa ajili ya Nuru ya Mungu.

Kumbuka, sanduku la agano lipo sasa ndani ya mioyo yetu! Sio tena kitu cha nje. Sisi ni hekalu la Mungu. Tafakari jambo hilo."Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?" (1 Kor 3:16).

**Yaliyomo katika Sanduku la Agano yanaashiria mambo makubwa matatu**

**Mana au Neno la Mungu**: Unapokuwa katika uwepo wa Mungu, Neno la Mungu lililofunuliwa huwa hai! Kama unao muda, hapa ni mahali pazuri sana pa kufungua Biblia yako na kumruhusu Bwana aseme nawe.

**Mbao za sheria**: Huu ni ukumbusho wa thamani kwamba sheria ya Mungu imeandikwa katika mioyo yetu. Siyo tena orodha ya mambo tunayopaswa kufanya au kutofanya.

**Fimbo ya Haruni**: Hii inamaanisha huduma yetu iliyopakwa mafuta ya kuwa watendakazi na mashujaa wa maombi kwa ajili ya Mungu. Kulikuwa na fimbo 12 zilizovunjika za mti wa mlozi zilizowekwa Hekaluni kwa amri ya Mungu. Fimbo mojawapo ambayo ingechipua kimiujiza wakati wa usiku, ingekuwa ile ambayo mmiliki wake ni mhudumu aliyechaguliwa na Mungu. Ni Mungu pekee

anayetupatia huduma, na tunatambua ni huduma gani pale tu tunapokuwa katika uwepo wake (Hesabu 17:8).

Hapa ndipo tunapoweza hasa kupokea ahadi za Mungu katika Neno lake. Tunapozipokea hapa, tunajua kwamba tutakuwa nazo!

Neno la Mungu katika wafilipi 4:19 linasema "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." Hapa unakuwa katika utukufu! Huu hapa utajiri wote wa mbinguni unakungojea.

Anza kumshukuru Mungu kwamba mambo haya matatu siyo tu kwamba yapo mbele zako, bali pia yako **NDANI** yako. Siyo tu kwamba yako **NDANI** yako lakini damu na kiti cha rehema na malaika wanakulinda kwa hayo. Katika Zaburi 91 tunasoma kwamba malaika zake watakulinda katika njia zako zote.

Sasa umeandaliwa kuwa mwombezi hasa. Unashiriki huduma ya Ukuhani Mkuu wa Yesu na kuwaombea wengine ipasavyo. Yesu alisema katika Yohana 15:7 "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."

**Huu unapaswa kuwa muda mzuri wa kustarehe na kufurahi katika uwepo wa Mungu.** Tumia muda wa kutosha hapa katika hali ya ukimya na kufurahia kuwa pamoja naye. Hupaswi hata kuongea. Mungu anafurahia jambo hili. Wewe pia utalifurahia. Jambo hili ndilo lililozungumzwa katika somo hili, yaani kuingia katika uwepo wa Mungu! Usisome tu jambo hili na kuendelea.

**Amua kabisa kwamba kila siku utafanya zoezi la kuingia katika uwepo wa Mungu.** Jambo hili ni muhimu sana ili kupata ushindi katika maisha haya na yale yajayo.

**Kiambatisho F**

## Kujichunguza Kiroho

- **Upendo -** Je unawatendea wengine kwa upendo wa Mungu usio na masharti?
- **Ubinafsi -** Kuweka mahitaji yako mwenyewe juu ya mahitaji ya wengine. Upendo hujishughulisha na ustawi wa mtu mwingine - je wewe unajijali mwenyewe zaidi na kujali tu jinsi unavyojisikia?
- **Kuiba** - Je unaweza kukumbuka fedha ulizopokea kwa mali iliyokuwa si yako?
- **Kulaghai** - Je, ulipata kitu chochote kutoka kwa mtu fulani kwa njia isiyo ya haki?
- **Kusema uongo -** Aina yoyote ya udanganyifu wa kukusudia
- **Kashfa** - Kumsema vibaya mtu fulani. Kumkashifu mtu siyo lazima useme uongo - Je, umewahi kuwasema wengine bila upendo?
- **Ufisadi** - Je, unajisikia hatia kuamsha tamaa usizoweza kuzitimiza kwa haki? Ufasiki, uchafu wote, hata kama ni juu ya mwili wako mwenyewe.
- **Ulevi -** Utumiaji wa madawa ya kulevya, karamu za ulevi.
- **Lugha chafu au matusi** - maneno maovu, mazungumzo mabaya au yasiyo na maana, uchafu, mazungumzo machafu, ya kipumbavu, ya kipuzi, ya upotovu.
- **Wivu** - Kwa kawaida mahali penye mazungumzo yanayohusu makosa au kushindwa kwa wengine, kuna wivu uliojificha.
- **Utovu wa shukrani** - Ni mara ngapi wengine wamekufanyia vitu lakini hukushukuru?
- **Hasira** - Je, umewahi kukasirika?
- **Kulaani** - Umetumia lugha ya matusi.
- **Utani** - Maneno yasiyohitajika, maongezi ya kipumbavu, kuongea na kutenda kama punguani. Masihara na mzaha na utani wa vitendo unaoelekea kudhoofisha viwango vitakatifu na vyenye thamani vya maisha. Je, umewahi kulitania kabila fulani au sehemu fulani ya

ulimwengu, taifa au mkoa katika nchi yako, au mwanasiasa fulani? Mizaha ya kikabila au kimikoa haina nafasi katika utakatifu.

- **Ukali** - Ulijibu mapigo, ulinung'unika au kurudisha mabaya kwa mabaya?
- **Tabia** - Je, kila wakati una uchu upitao kiasi? Na vipi kuhusu tabia yako ya ulaji?
- **Hali ya kuwa shingo upande** - Unaweza kukumbuka nyakati ambazo kwa makusudi kabisa ulikwepa kufanya wajibu wako kwa ukamilifu?
- **Kizuizi** - Umeharibu imani au matumaini ya wengine kwa kupoteza bure muda wao? Je, umemghilibu mtu aliyekuwa na imani na wewe?
- **Unafiki** - Je, maisha uliyoishi siku za nyuma, yamewafanya baadhi ya watu waone kwamba yale uliyoyasema juu ya Kristo na Injili yake ni ya uongo?
- **Kuvunja nadhiri** - Je, kuna nadhiri yoyote uliyoweka mbele za Mungu ambayo hukuitimiza?
- **Kutokusamehe** - Je, una kinyongo au uchungu dhidi ya mtu mwingine, rafiki au adui?
- **Mafarakano** - Misuguano, roho ya kuwa na vikundi vinavyotofautiana.
- **Kutamani**, kuishi kitajiri na kutapanya mali, ulafi. Kutumia pesa kupita kiasi kwa kununua vitu madukani. Kupoteza muda bure.
- **Kutowatendea** vyema, au kwa upendo na heshima, wake, waume, watoto na wazazi.
- **Kutoridhika**, kuwa na wivu kwa sababu wengine wana vitu lakini wewe huna.
- **Kuabudu sanamu** - Shauku yoyote katika maisha yako inayozidi shauku ya kuishi na Mungu.
- **Ugomvi** - Umechochea ugomvi kwa maneno yasiyohitajika?
- **Uchawi** - Kumtawala mwingine kwa hila ili kutimiza haja zako.
- **Kuasi mamlaka** - Mkuu wako wa kazi, mwalimu, mzazi, kiongozi wa kiroho, nk.
- **Kuupenda ulimwengu** - Pamoja na: tamaa za macho - unasoma au kutazama nini? Tamaa za mwili - unatamani nini? Kiburi cha uzima - Ni jambo gani katika maisha unalofikiri kwamba unaweza kulifanya bila Mungu kuhusika? - Kujifanya kuwa mkubwa au mdogo kuliko jinsi ulivyo kwa njia ya mawazo au kwa kuishi.
- **Kiburi** - ni dhambi kubwa kuliko zote. Chunguza maeneo haya.

- Je, unaangalia tu kushindwa au makosa ya wengine au unajishughulisha tu na mahitaji yako ya kiroho?
- Unajihesabia haki na kuwakosoa wengine au una huruma na moyo wa kusamehe, ukitafuta yaliyo bora kwa wengine?
- Je, unawaangalia wengine kwa dharau au unawaheshimu wengine wote na kuwaona bora kuliko wewe?
- Je, unajitegemea na kujitosheleza mwenyewe au unawategemea wengine na kutambua kwamba unawahitaji?
- Ni lazima udumishe hali ya kuwatawala wengine au uko tayari kuacha kutawala?
- Je, ni lazima uthibitishe kwamba uko sahihi, au uko tayari kuiachia haki ya kuwa sahihi?
- Una roho ya kuhitaji tu au roho ya utoaji?
- Unatamani kutumikiwa au una hamasa ya kuwahudumia wengine?
- Unatamani kupandishwa cheo au unafurahi wengine wanapopandishwa cheo?
- Unahitaji kupewa sifa au unafurahi wakati wengine wanapotambuliwa?
- Unasikia kujiamini kwamba unajua mengi, au yale ambayo bado hujajifunza yanakufanya uwe mnyenyekevu?
- Unajifahamu jinsi ulivyo au hujishughulishi na maisha yako kabisa?
- Unawaepuka watu au unatafuta kuwa karibu na wengine? Uko tayari kuchukua jukumu la kuwapenda watu kwa moyo?
- Unafanya haraka kuwalaumu wengine au uko tayari kukubali kuwajibika?
- Wewe ni mtu usiyetaka kukaribiwa na wengine au ni mtu rahisi kuwasikia wengine wanapokusihi?
- Wewe ni mtu unayejitetea unapokosolewa au unakubali kukosolewa kwa unyenyekevu na moyo mweupe?
- Unajishughulisha kutafuta kuheshimiwa au kuwa kama ulivyo?
- Unajishughulisha na yale ambayo wengine wanafikiri au yale anayofikiri Mungu?
- Unajitahidi kudumisha hali yako au hadhi uliyo nayo?
- Je, unaona vigumu kuwashirikisha wengine mahitaji yako ya kiroho au uko tayari kuwa wazi?
- Unajaribu kuficha dhambi zako au uko tayari kuonekana wakati unapokosea?
- Unajisikia tabu kusema, “Nilikosea, tafadhali nisamehe”?

- Unapoungama dhambi, unaungama kwa ujumla, au unakiri na kuzitaja kabisa dhambi zile ulizotenda?
- Unajutia dhambi zako unapokamatwa au unasikitika kwa kuzitenda na unafanya haraka kutubu?
- Wakati hali ya kutoelewana au migongano inapotokea, unangojea wengine waje kuomba msamaha au wewe ndiye unayeanza kufanya hivyo?
- Je, unajilinganisha na wengine na kujiona kwamba unastahili heshima au je, huwa unajilinganisha na utakatifu wa Mungu na kusikia hitaji kubwa la kupewa rehema?
- Je, unafikiri una mambo machache au huna kabisa mambo ya kutubu au kila siku una moyo wa toba?
- Je, unafikiri kila mtu anahitaji uamsho au kila siku unasikia hitaji la kupata upya ujazo wa Roho Mtakatifu?
- Unajivuna unapokaa na Mkristo mpya au unafurahia ari yake? Uko tayari kujifunza kutoka kwake?
- Je, unaogopa unapokaa na Mkristo aliyekomaa zaidi yako, au una njaa ya kujifunza mambo mbalimbali yanayotokana na uzoefu wake?

**Upasuaji unahitajika?**

**Iwapo Roho Mtakatifu anatuonyesha dhambi**, tunahitaji kwenda pale ambapo Bwana alikutana nasi kwa mara ya kwanza. Ni pale msalabani. Tunamuona Yesu akiwa amesulibiwa tena, kwa ajili ya dhambi hiyo, amebeba adhabu yetu.

**Damu inachuruzika chini kutoka msalabani.** Hali hiyo inapaswa kutushtusha na kutuhuzunisha kwa sababu tunaona hukumu ya Mungu ya kutisha. Tunahitaji kufahamu kwamba ghadhabu yote na hukumu ya Mungu iliwekwa juu ya Yesu msalabani.

**Yesu anatusubiri pale**, siyo kutuhukumu, bali anafurahi tukienda msalabani na kumpa dhambi zetu. Wakristo wengi wanapotambua dhambi humkimbia Mungu kwa aibu na kujisikia hatia.

**Dawa ya Mungu ya dhambi ni kwenda Msalabani**, kwenda Patakatifu pa Patakatifu katika uwepo wake na kuruhusu tabia yake itawale tabia yako. Utakatifu wake utaondoa dhambi zako. Hii pekee ndiyo dawa. Hatuwezi kufanya jambo hili sisi wenyewe. Ni kanuni ya kuondoa na kuweka. Hatuondoi dhambi zetu, Mungu ndiye anayetujaza utakatifu na upendo wake na dhambi lazima iondoke. Usikate tamaa iwapo inakubidi kufanya hivi mara kwa mara. Mungu hatuhukumu.

Anayefanya hivyo ni Shetani. Mungu atakukaribisha kila wakati utakapomwendea. Ukiacha kumwendea hapo ndipo anapohuzunishw.

**Tembea katika nuru ya kweli.** Acha kujidanganya, ikabili dhambi hii kama ilivyo. Iache kabisa kwa moyo wa dhati. Simama upande wa Mungu na kuipinga dhambi hiyo. Kusudia moyoni mwako kutoirudia KAMWE.

**Kuungama**:

**"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu** na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."(1 Yoh 1:9).

**"BWANA amejaa huruma na neema** Haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili. Yeye hatateta siku zote, wala hatashika hasira yake milele. Hakututenda sawasawa na hatia zetu, wala hakutulipa kwa kadiri ya maovu yetu; maana mbingu zilivyoinuka juu ya nchi, kadiri ile ile rehema zake ni kuu kwa wamchao. Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi." (Zaburi 103:8 - 12).

**Msamaha siyo tu kuondoa**. Msamaha ni neno zito linalomaanisha kukata na kuondoa kama daktari wa upasuaji anavyokata na kuondoa saratani. Msamaha wa dhambi unamaanisha kwamba dhambi imeondolwa kwako na kuwekwa kwa Yesu aliyeibeba msalabani.

**Kuungama ni kukubaliana na jinsi Mungu** anavyoliona jambo na kulitamka kwa kinywa chako. Kuungama siyo kutamka tamka tu, ni pamoja na kukubaliana na Neno. Unyenyekevu ni kukubali kwamba umekosea.

**Je, utafanya hivyo sasa?** Uko tayari kama mtoto mdogo kumwendea Baba yako mwenye neema na upendo na kungama dhambi zako na kuomba msamaha kwa unyenyekevu?

**"Ee Mungu, unajua upumbavu wangu**, wala hukufichwa dhambi yangu…kwa ajili ya jina lako, Unisamehe uovu wangu, maana ni mwingi…BWANA kama Wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama? Lakini kwako kuna msamaha, ili Wewe uogopwe.

Ee Mungu Baba yangu, nakuja mbele zako kuungama dhambi yangu (zangu) ya (za): (Sasa zitaje na kuziungama.)

Neno lako linasema kwamba matendo haya au mwenendo huu ni dhambi nami nakubaliana na Neno lako. Sina udhuru. Sitaki tena kufanya dhambi hii ndani ya roho, nafsi na mwili wangu. Nataka kuiacha na kutupa mbali nami. Inanitenganisha mimi na wewe. Inaniharibu. Nataka kuponywa, roho, nafsi na mwili, na pia nataka

kuwa karibu na wewe. Napokea msamaha wako. Asante kwa kuweka dhambi hii juu ya Yesu, na asante kwa kuwa aliiweka juu ya Msalaba wake kwa ajili yangu. Najua sistahili msamaha lakini nashukuru kwa kuniweka huru."

**Malipizo ni utayari** wa kulipa au kurudisha kitu fulani kila inapowezekana. Iwapo sasa umesamehewa mbele za Bwana , uko tayari kumwomba akupe ujasiri wa kuungama na kufanya malipizo kwa wengine uliowakosea? Ukitaka kuwa huru kweli kweli dhamiri yako lazima iwe safi mbele za Mungu NA wanadamu. Huwezi kumtetea Mungu huku unajiona mchafu mbele za macho ya watu wengine.

**Kumbukumbu za kushindwa kwako** mbele ya macho yao zitakuingiza ndani sana katika utumwa kila wakati unapowakumbuka. Kama hujawaomba msamaha, hali ya kujihisi una hatia itaiua imani yako na kukuibia mwelekeo na nia yako. Hata hivyo, hupaswi kuungama kila dhambi kwa kila mtu; ni dhambi zile tu ulizowatendea watu unaowajua.

**Kanuni**: Maungamo yanapaswa kufanywa kulingana na dhambi zilizotendwa. Kama ulitenda dhambi mbele za Mungu peke yake, Mungu atakusamehe na kusahau uliyoyatenda (Zaburi 103:8-13; Isaya 43:25; Yeremia 31:34). Dhambi ulizotenda mbele za Mungu na wanadamu ni lazima uzitubu mbele za wote WAWILI, Mungu na mtu (watu) uliyemkosea (uliowakosea).

Baadhi ya yale yaliyomo katika Kiambatisho F yalichukuliwa kutoka katika vijitabu vya Winkie Pratney vilivyochapishwa katika mtandao wa kompyuta (www)